**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**03** **MAARIFA YA JAMII**

**Muda: Saa 1:30** **MAJIBU** **Mwaka: 2022**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali manne (4).
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

SEHEMU A (Alama 28)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Jibu kipengele cha (i) – (viii) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku.

(i) Ni tukio gani la kihistoria lilitokea Tanganyika tarehe 9/12/1961?

A. Azimio la Arusha

B. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

C. Uhuru wa Tanganyika

D. Tanganyika kuwa Jamhuri

**C. Uhuru wa Tanganyika**

Tarehe 9 Desemba 1961 Tanganyika ilipata uhuru wake kutoka kwa Waingereza, hivyo tukio hilo ni Uhuru wa Tanganyika.

(ii) Zifuatazo ni faida za ngoma za asili isipokuwa:

A. Kuendeleza utamaduni

B. Kupata hamasa ya kufanya kazi

C. Kupata zawadi mbalimbali

D. Kufanya mwili kuwa na afya

**C. Kupata zawadi mbalimbali**

Kupata zawadi si faida ya moja kwa moja ya ngoma za asili, wakati zingine zinahusiana na afya, hamasa na utamaduni.

(iii) Lugha, mipaka, utamaduni na Serikali kwa pamoja huunda:

A. Taifa

B. Jamhuri

C. Bara

D. Raia


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

**A. Taifa**

Taifa huundwa na watu wanaounganishwa na lugha, utamaduni, mipaka na serikali.

(iv) Yupi ni msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

A. Spika

B. Rais

C. Waziri mkuu

D. Makamu wa Rais

**C. Waziri mkuu**

Waziri Mkuu ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za serikali bungeni.

(v) Yupi kati ya marais wa Tanzania alihusika katika kuanzishwa kwa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar?

A. Dkt. Jakaya M. Kikwete

B. Benjamin W. Mkapa

C. Samia Suluhu Hassan

D. Mwl. Julius K. Nyerere

**D. Mwl. Julius K. Nyerere**

Mwl. Julius K. Nyerere alihusika moja kwa moja katika kuanzisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964.

(vi) Kundi lipi hujumuisha familia ya watoto yatima?

A. Mama na watoto

B. Watoto bila wazazi

C. Watoto bila ndugu

D. Watoto wa mtaani

**B. Watoto bila wazazi**

Watoto yatima ni wale waliopoteza wazazi wao.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

(vii) Zifuatazo ni aina za ukabaila zilizokuwepo Tanzania, isipokuwa:

A. Umwinyi

B. Ubugabire

C. Nyarubanja

D. Ujamaa

**D. Ujamaa**

Ujamaa ni mfumo wa kijamaa, si aina ya ukabaila.

(viii) Mfumo upi wa uzalishaji mali ambao jamii zote zimepitia?

A. Ubepari

B. Ujamaa

C. Ujima

D. Ukabaila

**C. Ujima**

Ujima ni mfumo wa kwanza wa uzalishaji mali ambao jamii zote za binadamu zilipitia.

2. Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha matumizi ya kifaa kinachotumika kufanya usafi maeneo ya shule katika Fungu A na aina ya kifaa husika katika Fungu B.

(i) Kukata miti mikubwa na matawi

**B. Shoka**

(ii) Kupunguza matawi ya miti

**G. Panga**

(iii) Kupalilia

**D. Jembe**

(iv) Kukusanya takataka

**H. Reki**

(v) Kubeba takataka

**E. Toroli**

(vi) Kuondoa tandabui

**A. Dekio**

SEHEMU B (Alama 22)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Wilaya yetu ina utajiri mwingi unaotokana na maliasili tulizonazo. Maliasili hizi huwezesha kufanyika kwa shughuli nyingi za kiuchumi ambazo huingizia wilay yetu fedha nyingi. Tuna mto na bahari ambapo samaki huvuliwa kwa ajili ya chakula na biashara.

Uvuvi wa kwenye mto huitwa uvuvi wa maji baridi na samaki wake huitwa samaki wa maji baridi. Uvuvi unaofanyika baharini huitwa uvuvi wa maji chumvi na samaki wake huitwa samaki wa maji chumvi. Uvuvi huwapatia wakazi ajira na fedha. Njia mbalimbali hutumika katika uvuvi kutegemea eneo na aina ya samaki. Kuna uvuvi wa kutumia nyavu au ndoano.

Wavuvi wanaotumia wavuhupata samaki wengi zaidi kuliko wale wanaotumia ndoano. Wavu ukiwa na matundu madogo huwa na athari kwani huvua samaki wakubwa na wachanga. Samaki wachanga wakivuliwa eneo hilo litakosa samaki siku za baadae.

(i) Rasilimali zina faida gani?

Rasilimali **huwezesha kufanyika kwa shughuli za kiuchumi na kuingiza fedha**.

(ii) Taja faida moja ya uvuvi.

Faida moja ya uvuvi ni **kupata ajira na chakula**.

(iii) Ni aina gani ya samaki huvuliwa katika mto?

Katika mto huvuliwa **samaki wa maji baridi**.

(iv) Ni aina ipi ya uvuvi hufanyika baharini?

Bahari hufanyika **uvuvi wa maji chumvi**.

(v) Ni athari ipi husababishwa na uvuvi wa samaki wachanga?

Athari ni **kupungua au kuisha kwa samaki siku za baadaye**.

(vi) Ni njia ipi ya uvuvi hutupatia samaki wengi?

Njia inayotupatia samaki wengi ni **uvuvi wa kutumia nyavu**.

(vii) Ipi ni athari ya kuvua samaki kwa kutumia wavu wenye matundu madogo?

Athari ni **kuvuliwa samaki wakubwa na wachanga na kuharibu mazalia ya samaki**.

4. Wanafunzi wa Darasa la Nne walitakiwa kuchora ramani ya shule yao. Ni vipengele vipi vya ramani wanapaswa kuzingatia wakati wa kuchora ramani? Bainisha vipengele vine.

Kipengele cha kwanza ni **kichwa cha ramani**, ambacho huonyesha ramani inahusu nini.

Kipengele cha pili ni **alama au ufunguo wa ramani**, unaosaidia kutafsiri alama zilizotumika.

Kipengele cha tatu ni **mwelekeo wa ramani**, unaoonyesha upande wa kaskazini, kusini, mashariki na magharibi.

Kipengele cha nne ni **uwiano au kipimo**, kinachoonyesha uhusiano kati ya umbali halisi na ule uliopo kwenye ramani.